# WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI

SHULE YA SEKONDARI NDANDA

S.L.P. 10
NDANDA

**Simu: 0783625463**

---

KUMB. NA. NSS/A.12/2022 05/04/2022

NDG. MZAZI/MLEZI WA
-----------------------------------------------------
-----------------------------------------------------

YAH: **MAELEKEZO YA MWANAO KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO (V) KATIKA SHULE YA SEKONDARI NDANDA**

Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu.

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao ------------------------------------------- ni miongoni mwa vijana wachache waliopata bahati/fursa ya kuendelea na masomo ya kidato cha tano katika shule ya sekondari Ndanda – Hongera sana.

Kwa barua hii nakuletea fomu ya kujiunga shule ya sekondari Ndanda kwa mwanao. Tafadhali nakuomba wewe na mwanao msome maelekezo haya kwa kina na kisha mkamilishe yale yote yanayotakiwa.

Pamoja na kuyasoma kwa kina naomba uendelee kumshauri mwanao juu ya kutumia nafasi hii aliyoipata vema ili lengo na azma yake itimie.

Nakutakia maandalizi mema na karibu sana Ndanda Sekondari.

Wako

PATRICK N. NDUNGURU
**MKUU WA SHULE**

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI

SHULE YA SEKONDARI NDANDA

**SIMU NA. 0783625463**

S.L.P. 10
NDANDA

---

KUMB. NA. NSS/A.12/ 2022 05/04/2022

Ndg. Mzazi/Mlezi wa

---------------------------------------------------

---------------------------------------------------

----------------------------------------------------

YAH: **<u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE</u>**

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao …………………………………….. amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano (V) kwa mchepuo wa ………….. katika shule ya sekondari Ndanda. Anatakiwa aripoti shuleni tarehe **……….** akiwa amekamilisha yale yote aliyoelekezwa katika fomu hii.

Ndanda sekondari ipo katika mji mdogo wa Ndanda uliopo Wilaya ya Masasi katika Mkoa wa Mtwara. Kwa wanaotoka mikoani kupitia Dar es Salaam usafiri wa kuja Ndanda unapatikana kituo kikuu cha mabasi Mbezi Loius (Kituo cha mabasi cha Magufuli), uliza mabasi yaendayo Masasi na shuka kituo cha Ndanda. Kwa walioko mikoa ya Nyanda za Juu Kusini watatumia usafiri wa barabara kupitia Songea, Tunduru hadi Masasi na kufika Ndanda.

Shule ipo upande wa Mashariki umbali wa Kilomita mbili (2KM) kutoka kituo kikuu cha mabasi Ndanda. Shule ina mazingira mazuri na huduma zote muhimu zinapatikana kwa uhakika. Karibu sana Ndanda sekondari.

## ***<u>MAELEKEZO/MAAGIZO NA MASHARTI YA KUJIUNGA NA SHULE</u>***

Ili mwanao apokelewe shuleni, anatakiwa afanye yafuatayo:-

1. Apimwe katika Hospitali inayotambulika ya serikali na fomu iliyoambatanishwa kujazwa na Mganga/Daktari mhusika.
2. Aje na hati ya matokeo yake ya kidato cha nne (Result slip), nakala ya cheti cha kuhitimu kidato cha nne (Leaving certificate) na ikiwezekana na nakala ya cheti cha kuzaliwa.
3. Aje na bima ya Afya **(NHIF**), kwa wanafunzi ambao hawana bima ya Afya waje na kiasi cha Tsh. 50,400/= ambayo itamsaidia kupata bima awapo shuleni. ***NI LAZIMA AWENAYO***

4. ***SARE ZA SHULE*:**

- Suruali mbili (02) za rangi ya damu ya mzee (Esteem namba 1, yenye turn up chini na upana inchi 16 yenye marinda juu) **na kama haitakidhi vigezo vilivyoainishwa haitapokelewa.**
- Mashati mawili (02) meupe mikono mirefu
- Viatu vya ngozi vyeusi vyenye visigino vifupi vyenye kamba (sio raba)
- Sweta rangi ya damu ya mzee lenye shingo "V" (makoti hayaruhusiwi)
- Soksi nyeusi jozi (pair) tatu.

***4. SARE/NGUO ZA KAZI***

- Suruali nyeusi mbili (2) ziwe na turn up (inchi 16) ziwe na marinda
- Fulana ya bluu yenye kola (Form six blue plain isiyo na maandishi).
- Raba za rangi yoyote
- Nguo za michezo (Track Suit ya Rangi ya Dark Blue)

**NB:** ***Nguo zingine tofauti na zilizo ainishwa katika fomu hii haziruhusiwi na hivyo mwanafunzi hatakiwi kuja nazo*.**

***5. ADA NA MICHANGO MBALIMBALI YA SHULE:***

Ada na michango yote ilipwe bank na mwanafunzi aje na hati ya malipo (Bank slip).

***(i)*** Ada – Tsh. 35,000/= kwa muhula na Tsh. 70,000/= kwa mwaka. Ada ilipwe kwenye Akaunti Na. 70501200115 iliyopo NMB. Jina la Akaunti ni ***SHULE YA SEKONDARI NDANDA.***

***(ii)*** Kiasi cha Tsh. 118,000/= kama michango ya mwaka mzima. kilipwe katika akaunti Na. 70501200169 iliyopo NMB. Jina la akaunti ni ***SHULE YA SEKONDARI NDANDA*** iliyopo NMB. Hata hivyo bado michango hiyo unaweza ukailipa kwa awamu yaani muhula wa kwanza Tsh. 91,000/= na muhula wa pili Tsh. 27,000/=.

Mchanganuo wa kiasi hicho ni kama ifuatavyo:-

| S/NA | MCHANGO | MALIPO YA MUHULA I | MALIPO YA MUHULA II | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 01 | Taaluma | 10,000/= | 10,000/= | 20,000/= |
| 02 | Ukarabati | 15,000/= | - | 15,000/= |
| 03 | Huduma ya kwanza | 10,000/= | | 10,000/= |
| 04 | Malipo kwa vibarua i.e wapishi, walinzi n.k. | 20,000/= | 7,000/= | 27,000/= |
| 05 | Kitambulisho cha shule | 6,000/= | - | 6,000/= |
| 06 | Nembo | 2,500/= | - | 2,500/= |
| 07 | Mtihani wa kujipima (mock) | 10,000/= | 10,000/= | 20,000/= |
| 08 | Kukodi godoro | 10,000/= | | 10,000/= |
| 09 | Tahadhari | 5,000/= | - | 5,000/= |
| 10 | UMISETA | 2500/= | | 2,500/= |
| **JUMLA** | | **91,000/=** | **27,000/=** | **118,000/=** |

**(iii) Kwa wanafunzi ambao hawana bima ya Afya wanatakiwa waje na Tsh. 50,400**

### *6. MAHITAJI MENGINEYO:*

Aidha anatakiwa awe na vitu vifuatavyo:- ( Alama ***** hiyo inamaanisha kifaa hicho kinapatikana katika duka la shule kwa gharama zilizoainishwa kwenye jedwali la chini).

(i) *Shuka mbili rangi za bluu bahari (Light blue) mto na foranya, na taulo.

(ii) Sanduku imara la kuweka vitu vyake.

(iii) *Sahani, Bakuli, Kijiko na kikombe

(iv) *Ndala za kuogea.

(v) *Daftari 12 – counter book Quire 3/Quire 4.

(vi) Mathematical set, scientific calculator kwa wanafunzi wa michepuo ya PCM, PCB, CBG, PGM, EGM na HGE (Calculator iwe na ROM ya 12)

(vii) Rimu mbili ya karatasi – A4, moja muhula wa kwanza na nyingine muhula wa pili.

(viii) *Dawa za chooni:

- Toilet Deodarant moja (Toilet balls)
- Dawa ya maji ya kusafishia choo aina ya ARO

(ix) Fyekeo kwa CBG, PCB, PCM na HGL, Panga kwa HGE, Jembe lenye mpini kwa HKL, HGK, PGM na EGM.

(x) Chandarua cha pande nne na sio cha mviringo kwa juu.

(xi) *Ndoo mbili zenye ujazo wa lita kumi kila moja.

(xii) *Fagio (soft broom) na drier (mopa) kwa CBG,PCB, HKL na HGL

*Fagio (hard broom) na drier (mopa) kwa HGK,HGE, EGM, PCM, PGM.

(xiii) *File mbili

(xiv) Graph pad moja kwa mwanafunzi wa PCM/PCB/PGM/CBG/EGM/HE/HGK na HGL

(xv) Jozi moja ya raba kwa ajili ya mazoezi.

(xvi) *T – shirt moja ya shule.

NB: **Huduma/Mahitaji yafuatayo yanapatikana shuleni kwenye duka la shule. Hivyo ni vema ukajua gharama/bei ya vitu hivyo viliyoorodheshwa hapa chini:-**

| S/N | HITAJI | IDADI HITAJIKA | BEI @ KWA MOJA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Shuka za Bluu | 2 | 8,000/= | 16,000/= |
| 2 | Sahani, Bakuli, kikombe na kijiko | Vyote vinne | | 3,500/= |
| 3 | Daftari za counter book (Quire 4) | 12 | 4,500/= | 54,000/= |
| 4 | Dissecting Kit (kwa wanafunzi wanaochukua Biology) – CBG & PCB | 1 | 35,000/= | 35,000/= |
| 5 | Rimu ya karatasi A.4 | 2 | 14,000/= | 28,000/= |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6 | Dawa za chooni<br>▪ ARO<br>▪ Toilet deodarant | <br>1<br>1 | <br>6,000/=<br>3,500/= | <br>6,000/=<br>3,500/= |
| 7 | Fagio<br>➢ Soft broom - (kwa wanafunzi wa mchepuo wa CBG, PCB, PCM,HKL na HGL)<br>➢ Hard Broom (kwa wanafunzi wa EGM, PCM, HGE, HGK na PGM) | 1<br>1 | 3,000/=<br>3,000/= | 3,000/=<br>3,000/= |
| 8 | ➢ Graph pad | 1 | 3,500/= | 3,500/= |
| 9 | Suruali mbili (02) za shule rangi ya damu ya mzee (Esteem one ) | 2 | 20,000/= | 40,000/= |
| 10 | Tai | 1 | 4,000/= | 4,000/= |
| 12 | T – shirt moja (01) ya shule | 1 | 12,000/= | 12,000/= |

***ZINGATIA:***

(i) Tafadhali, mwanao asome sheria, kanuni na taratibu za shule na kama yuko tayari kufuata taratibu husika akiri mbele yako kwa kujaza fomu husika zilizoambatanishwa.

(ii) Mwanafunzi atakae chelewa na kufika shuleni zaidi ya tarehe …………… ***hatapokelewa***. Hivyo ni vema ukamwandaa mapema mwanao na akafika mapema shuleni. Wanafunzi wa kidato cha tano wataanza kuingia darasani na kufundishwa kuanzia wiki ya kwanza ya kuripoti shuleni aidha watafanya mtihani/jaribio la kwanza kuanzia wiki ya nne baada ya kuripoti shuleni.

***(iii) NI MARUFUKU MWANAFUNZI KUJA NA SIMU SHULENI. IWAPO MWANAFUNZI ATABAINIKA/ATAKAMATWA NA SIMU ATAFUKUZWA SHULE***

Tafadhali, mwanao afike shuleni na barua hii na ajaze kwa ukamilifu sehemu ya

taarifa maalum kwa mwanafunzi mpya.

Nakutakia maandalizi mema na safari njema ya kuja Ndanda.

*KARIBU SANA* `

PATRICK N. NDUNGURU
**MKUU WA SHULE**

***NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambae ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFAHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA:-***

- ***Mkuu wa shule - 0783625463 au 0621811009***
- ***Makamu Mkuu wa Shule 0714998228au 0782478667***

- ***Mwandamizi Taaluma - 0716 68 03 99***
- ***Mwandamizi Malezi - 0717401017/0753553325 au 0756513453***

**SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

TO THE MEDICAL OFFICER

---------------------------------------------------
---------------------------------------------------
---------------------------------------------------

Name of student ---------------------------------------------------------------------------------------
Form ---------------------------- Term --------------------------- Year ---------------------------

Dear Doctor

Please kindly examine the above named student to prove his/her fitness undertaking studies at our school.

1. X-ray ( ) 2. Urine ( ) 3. Stool ( )

4. Physical fitness ( ) 5. V.D ( ) 6. Tuberculosis ( )

**A: (I) PRELIMINARY INFORMATION (BY THE STUDENT BEFORE THE DOCTOR)**

| NO | DISEASE | YES/NO | NO | DISEASE | YES/NO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tuberculosis | | 10 | Epilepsy | |
| 2 | Pneumonia | | 11 | Ear, Nose and threat | |
| 3 | Asthma | | 12 | Skin disorder disease | |
| 4 | Heart trouble | | 13 | Anemia | |
| 5 | Recurrent indigestion | | 14 | Operations | |
| 6 | Jaundice | | 15 | Serious Accident | |
| 7 | Dysentery | | 16 | Malaria | |
| 8 | Kidney and urinary trouble | | 17 | Stomach trouble | |
| 9 | Nervous breakdown | | 18 | Eye disorder | |

**(II) VACCINATIONS AND INNOVULATIONS HISOTRY**

| DISEASE | 1ST DATE | 2ND DATE | 3RD DATE |
|---|---|---|---|
| Small pox | | | |
| Whooping cough | | | |
| Measles | | | |
| Yellow fever | | | |
| Cholera | | | |

**Official**

**B: MEDICAL EXAMINATION REPORT**

(a) Weight

(b) Heat Beat

(c) Vision etc

**MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the above and consider that he/she is physically fit/unfit to undergo studies.

DOCTOR’S NAME & SIGNATURE -------------------------------------------------------------------------------

DATE ------------------------------------

**SHULE YA SEKONDARI NDANDA**

**TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

**SEHEMU A:**

Jina la Mwanafunzi --------------------------------------------------------------------------------

wa kidato cha V Mchepuo wa -------------------------- Mwaka --------------------------------

Dini ……………………………………………………………………………………….

**ELIMU:**

(i) Shule ya Msingi niliyosoma ni --------------------------- iliyoko -----------------------------

Wilaya ya ------------------------------------- Mkoa wa -----------------------------------------

Kuanzia mwaka ----------------------------- Mpaka ---------------------------------------------

**SEHEMU B: TAARIFA ZA WAZAZI/WALEZI NA JAMAA:**

**(i)** Baba anaitwa ------------------------------------------------------------------------------------

Anaishi kijiji/mtaa ------------------ Kata ------------- Wilaya-------------Mkoa------------

Kazi yake ni ---------------------------- na anwani yake ni -----------------------------------

----------------------------------------------------------------------------------------------------------

Namba yake ya simu ni ----------------------------------------------------------------------

(ii) Mama anaitwa ------------------------------------------------------------------------------------

Anaishi kijiji/mtaa ------------------ Kata ------------- Wilaya-------------Mkoa------------

Kazi yake ni ---------------------------- na anwani yake ni -----------------------------------

----------------------------------------------------------------------------------------------------------

Namba yake ya simu ni ----------------------------------------------------------------------

**NDUGU ZANGU WENGINE:**

(iii) Jina ------------------------------------------------------------------------------------------------

Uhusiano ------------------------------------------------------------------------------------------

Kazi yake -------------------------------------------------------------------------------------------

Anaishi kijiji/mtaa ----------------------------- Kata ya -------------------------------------

Wilaya ya ------------------------------------ Mkoa wa ---------------------------------------

Namba yake ya simu ni ------------------------------------------------------------------------

(iv) Jina ---------------------------------------------------------------------------------------------

Uhusiano ---------------------------------------------------------------------------------------

Kazi yake ------------------------------------------------------------------------------------

Anaishi kijiji/mtaa -------------------------------- Kata ya ------------------------------------

Wilaya ya ----------------------------- Mkoa wa ----------------------------------------------

Namba yake ya simu ni ------------------------------------------------------------------------

(v) Jina ---------------------------------------------------------------------------------------------

Uhusiano ---------------------------------------------------------------------------------------

Kazi yake -------------------------------------------------------------------------------------

Anaishi kijiji/mtaa ------------------------------- Kata ya ---------------------------------------

Namba yake ya simu ni --------------------------------------------------------------------------

Mimi --------------------------------------------------------------- ambae ni mwanafunzi wa kidato cha V Mchepuo wa -------------------------- katika mwaka wa masomo --------------- nathibitisha kuwa maelezo yote niliyoyatoa hapo juu ni ya kweli na sahihi.

**SEHEMU C: UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI:**

Mimi ------------------------------------------------------------- nakiri kuwa nimezisoma Sheria, Kanuni na Taratibu za shule kwa umakini na utulivu mkubwa. Hivyo basi ninaahidi:

"Nitazifuata Sheria, Kanuni na Taratibu za shule kama zilivyoelekezwa. Aidha ninaamini kuwa Sheria na Taratibu zote zipo kwa nia ya kunisaidia katika nyanja zote muhimu ikiwa ni pamoja na nidhamu na taaluma".

Kinyume na hivyo hatua stahiki za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu.

Jina la Mwanafunzi ----------------------------------------- Sahihi ----------------------

Jina la mzazi/mlezi -------------------------------------------- Sahihi ----------------------

Tarehe ----------------------

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI

SHULE YA SEKONDARI NDANDA

## SHERIA ZA SHULE

Zifuatazo ni sheria za shule kinyume nazo kutasababisha mwanafunzi kuadhibiwa, kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule kabisa.

### MAKOSA YA KUFUFUKUZWA SHULE:

1. Wizi
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
3. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
4. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
5. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
6. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
7. Kufuga ndevu.
8. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
9. Uvutaji wa sigara.
10. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
11. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
12. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
13. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
14. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
15. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
16. Kudharau Bendera ya Taifa.
17. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
18. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

### MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUADHIBIWA:

1. Kutosimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri anapopita, kuingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano na mahali pengine popote.
2. Kuvaa viatu vyovyote vya mikanda vikiwemo kandambili, ndala n.k.
3. Kutumia lugha chafu dhidi ya wanafunzi wenzake, kwa walimu au mtu mwingine yeyote.
4. Kutovaa sare sahihi mf. Modal trousers na ipasavyo.
5. Kutowaheshimu wafanyakazi wote waliopo shuleni kama walezi wake.

6. Kutoonyesha dhamira ya kusaidia na kushiriki katika kazi kwani kazi ni kielelezo cha utu.
7. Kutoheshimu au kutothamini kazi za aina zote zinazotolewa na uongozi wa shule.
8. Uvutaji sigara
9. Kufuga ndevu
10. Kuvaa mavazi yasiyo na heshima
11. Kutotii kengele au kushindwa kuitikia mwito wa kiongozi aliyemuita
12. Kutoheshimu picha za viongozi wa serikali, nembo ya taifa “Coart of Arms” wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
13. Kutosimama katika utaratibu maalum wakati wa kupokea huduma.
14. Kutoheshimu na kutokubali tofauti za kisiasa, kidini na kiutamaduni.
15. Kutohudhuria vipindi vya madarasani kwa muda wote wa masomo
16. Kutohudhuria kazi zote za mikono, mikutano yote ya shule,, ukaguzi na usafi, kupandisha bendera ya taifa n.k.
17. Kushindwa kuthamini muda.
18. Kutowahi katika shughuli zote kama zilivyopangwa ukiwemo wito wa dharura.
19. ***Kutovaa sare za shule katika sehemu zifuatazo***:

    (a) Darasani

    (b) Shughuli za kishule nje ya shule

    (c) Mhadhara wa shule (School Baraza)

    (d) Kwenda kutibiwa hospitalini

    (e) Kwenye maandamano yaliyo rasmi

    (f) Anaposafiri kwenda na kurudi likizo
20. Kuvaa kofia, viatu vya gorofa na kandambili, (yeboyebo) na mapambo yo yote kwa mfano pete, mkufu na rozari.
21. Kutokuwa msafi katika mwili na nguo
22. Kutoheshimu mipaka ya shule
23. ***Marufuku kuingia sehemu zifuatazo bila ruhusa***:

    (a) Ofisi ya walimu (Staffroom)

    (b) Ofisi za shule

    (c) Maabara

    (d) Jikoni

    (e) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu

24. ***Sehemu zifuatazo ni marufuku kabisa kutembelea***;

(a) Vilabu vya pombe

(b) Kumbi/nyumba za starehe

(c) Nyumba za kufikia wageni (Guest Houses)